

## **Mwandishi Mtanzania Erick Kabendera aachiwa huru, lakini anakabiliwa na faini kubwa**

Nairobi, 25 Februari, 2020 -- Kamati ya Kuwalinda Wanahabari (CPJ) imekaribisha habari za kuachiwa huru kwa mwandishi wa kujitegemea Mtanzania Erick Kabendera lakini imesitikishwa sana na faini kubwa ambayo ametozwa.

Jana, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu jijini Dar es Salaam iliridhia makubaliano kati ya mwandishi huyo na upande wa mashtaka ya kukiri makosa na ikamwachia huru Kabendera. Mwandishi huyo alikuwa amezuiliwa tangu Julai 29, 2019 akikabiliwa na mashtaka ya ukwepaji kodi, utakatishaji wa fedha na kuongoza genge la uhalifu, kwa mujibu wa [taarifa](#) ya BBC Swahili na [vyombo vya habari](#) nchini humo. Chini ya makubaliano hayo, Kabendera alikiri makosa ya ukwepaji kodi na utakatishaji fedha, lakini kosa la genge la uhalifu likaondolewa, na akapigwa faini ya shilingi za Kitanzania 273 milioni (\$118,000), kwa mujibu wa taarifa hizo.

“Tunakaribisha kuachiwa huru kwa Erick Kabendera baada ya kuwa kizuizini karibu miezi saba, kwa mashtaka ambayo ilikuwa wazi yalikuwa ya kulipiza kisasi dhidi uandishi wake,” amesema mwakilishi wa CPJ kusini mwa Jangwa la Sahara-Muthoki Mumo. “Hata hivyo, tunasikitishwa sana kwamba hata baada ya kuzuiliwa kwa miezi mingi hivyo bila uwezekano wa kupewa dhamana, kipindi ambacho aliugua na kufiwa na mamake, mahangaiko ya Kabendera bado hayajafikia kikomo kwani faini hiyo kubwa itaendelea kumsumbuu.”

Mahakama ilimwamuru Kabendera kulipa faini ya shilingi 100 milioni za Kitanzania (\$43,000) kwa kosa la utakatishaji fedha, na faini ya shilingi 250,000 (\$108) kwa kosa la ukwepaji kodi, na pia aliye shilingi 173 milioni (\$75,000) kama fidia kwa kodi ambayo inadaiwa alikwepa kulipa, kwa mujibu wa BBC na Jebra Kambole, wakili wa mwandishi huyo, aliyezungumza na CPJ kupitia mtandao wa mawasiliano wa kijamii.

Gazeti la kibinagsi la *Mwananchi* liliripoti kuwa Kabendera tayari amelipa faini hiyo ya utakatishaji fedha, na Kambole aliambia CPJ kuwa mwandishi huyo alilipa faini ya shilingi 250,000 ya kosa la ukwepaji kodi jana. Anatakiwa kulipa fidia iliyosalia ya ukwepaji kodi katika kipindi cha miezi sita, kwa mujibu wa BBC na taarifa ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC).